**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**KISWAHILI 102/2**

1. UFAHAMU

(a) Anaonyesha kuwa wazazi wana jukumu la kuwashauri na kuwaelekeza vijana kwa njia iliyo wazi na pasipo na kuwaachia wengine. (2x1)

(b) Kupata mimba isiyostahiki.

Kuwaambukiza ugonjwa hatari wa ukimwi.

Maradhi mengine ya zinaa huyapata.

Kupotoka kimaadili. (zozote 4x1)

(c) Hawana wakati wa kukaa na kuwalea watoto wao.

Hushughulikia masuala ya kuleta riziki na kuwaacha watoto pekee.

Hukwepa malezi kwa kuwapeleka watoto shule za malezi mapema.

Kushiriki ilevi vilabuni eti wanakutana na marafiki.

Kupotoka kimaadili hasa mavazi yao. (zozote 4 x 1)

(d ) kulipia mtoto karo

Kununua chakula

Kuwanunulia watoto mavazi

Kuwapa watoto pesa za masrufu (mfukoni)

Kuwaelekeza watoto wao mara kwa mara (zozote 3 x 1)

(e) (i) Habari ambazo hazijadhibitishwa/visababu/kushikilia wanalosema ni kweli. (alama1x1)

( ii) kama tangazo la kutoa tahadhari. (alama1x1)

2. UFUPISHO

(a) Manufaa ya runinga

Ni nyenzo mwafaka ya kufundisha

Huleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani.

Ikitumika pamoja na video hufanya na kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha.

Ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku.

Hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii.

Ni kioo kinachoakisi mikakati na amali za jamii. (alama 7)

(b ) Runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili.

Huwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia: tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi.

Hueneza maadili yasiyofaa mathalan, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa.

Huhimiza matumizi ya madawa ya kulevya ambayo huwavutia vijana na watoto wengi.

Ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi kupitia vibonzo.

(alama 5) ( ALAMA 3 ZA MTIRIRIKO ZITUZWE KWA JUMLA)

3 . MATUMIZI YA LUGHA

(a) Ni kipashio cha utamkamji ambacho hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti.

AU

Ni sauti moja au zaidi zinazotamkwa kama fungu moja la sauti/kama sauti moja. (1x 2)

(b) Msichana alitoka darasani polepole/taratibu/asteaste. (2 x 1)


(c) A-li-ye-m- viambishi awali (alama 2)

i-a - viambishi tamati (alama 1)

(d) "Sikiliza bwana mdogo. Siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika. Hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote." Alifoka Abdi./

"Sikiliza bwana mdogo, siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika. Hayo mawazo yako ya zama kongwe hayatakufikishapopote," alifoka Abdi.

(e)




½ x8 =4

(f) (Nyumba) iliyojengwa jana – kishazi tegemezi (alama 1)

Nyumba imebomolewa - kishazi huru (alama 1)

(g) (i) fa- fia. Yesu alitufia msalabani. (alama 1)

(ii) soma- somesheana. Juma na Hamisi walisomesheana watoto. (alama 1)

(h) Mara kadha- kielezi cha idadi (alama 1)

Mwaka jana- kielezi cha wakati (alama 1)

(i) Mtoto – shamirisho kitondo

Vitabu – shamirisho kipozi

Mkoba – shamirisho ala (3 x 1)

(j) Amekuwa – kitenzi kisaidizi (Ts)

akilala - kitenzi kikuu (T)

yu - kitenzi kishirikishi (t) (3 x 1)

(k) /t/ - sighuna

/d/ - ghuna (½ x4)

(l) Amegura- amehama/ amehajiri

Mvulana – ghulamu/barubaru/barobaro/kinda (2 x 1)

(m) Amenivunjia mlango na kuniibia/akaniibia. (2 x 1)

(n) Kamati – nomino ya jamii ngeli ya I-ZI ( ½X 2)

Werevu – nomino ya dhahania ngeli ya U-U (½X 2)

(lazima aonyeshe nomino kwanza)

(o) Aliinua mkono ili gari lisimame/limbebe- mtu mwingine alikuwa anaendesha gari.

Aliegesha gari njiani –alikuwa anaendesha gari.

Alipiga gari breki njiani. ( 2x 1)

(p) "na" ya pamoja na au kiunganishi

" na" ya wakati (uliopita)

"na" ya mtenda ( 3 x 1)

(q) Mwenye kitabu aniazime.

Mwenye pesa anikopeshe.

( nomino inayorejelewa isitajwe) (1x 1)

**4. ISIMU JAMII**

(a) SABABU ZA WATU KUCHANGANYA MSIMBO

Athari za lugha zote

Kukosa msamiati wa kutumia

Upungufu wa kimsamiati katika lugha moja

Kuficha ujumbe

Kutaka kuonyesha ujuzi katika lugha nyingi

Kutaka kushirikisha watu katika mazungumzo

Mazoea

Mtu anapokuwa na hasira,mshtuko au furaha. (zozote 5 x1)

(b )

i. Matumizi ya ukale wa lugha km.Abraham akamjua Sara wakapata mwana.
ii. Matumizi ya msamiati maalum k.v sadaka, Mungu asifiwe,Alhammdulilahi.
iii. Matumizi ya sentensi ndefu.
iv. Kunukuu vifungu vya maandiko matakatifu.
v. Uradidi /urudiaji wa maneno.
vi. Kuonyesha hali ya udhaifu wa binadamu akilinganishwa na Mungu km.Mungu anajua yote.
vii. Matumizi ya ishara na miondoko.
viii. Kuchanganya nyakati.
ix. Kuboronga /kuharibu sarufi.
x. Matumizi ya maneno yenye asili ya kigeni/ ya zamani k.m kanani.